**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

# YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................................................ 1

2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ............................................ 6

2.1.1 Maoni na ushauri wa Kamati uliotekelezwa na Serikali . 6

2.1.2 Ushauri wa Kamati unaoendelea kutekelezwa ............ 11

2.1.3 Ushauri wa Kamati ambao haujatekelezwa ................. 13

3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.......... 15

3.1 Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12 ............... 17

3.2 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu 16......... 19

3.3 Divisheni ya Mashitaka (DPP) - Fungu 35...................... 21

3.4 Mfuko wa Mahakama - Fungu 40 .................................. 23

3.5 Wizara ya Katiba na Sheria – Fungu 41 ........................ 27

3.6 Tume ya Kurekebisha Sheria- Fungu 59 .......................... 29

3.7 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55 .......................................................................... 31

3.8 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency*-RITA)...................... 33

4.0 HITIMISHO ........................................................................ 35

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni 99 (5), (9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba kama ifuatavyo:-

i) Fungu 12-Tume ya Utumishi wa Mahakama;
ii) Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
iii) Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka;
iv) Fungu 40- Mahakama;
v) Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria;
vi) Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na
vii) Fungu 59- Tume ya Kurekebisha Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 4 Mei, 2015 Kamati yangu ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2014/2015.

***Mheshimiwa Spika***, Ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, baadhi ya mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

i) Uhusiano baina ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na mipango iliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015;

ii) Uhusiano baina ya dhima na dhamira na namna malengo yalivyotekelezwa;

iii) Uhusiano baina ya fedha zilizotengwa kwa mipango ya Wizara na taasisi zake pamoja na fedha zilizopatikana kutoka Hazina;

iv) Uhusiano uliopo kati ya fedha zilizopatikana na malengo yaliyotekelezwa;

v) Uwiano wa fedha zilizotumika ikilinganishwa na fedha zilizopatikana na kubaki hadi mwezi Machi, 2015; na

vi) Azma ya Serikali katika usimamiaji wa haki na utawala wa sheria.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015


**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 30, 2015 Wizara ilipokea jumla ya Shilingi (Tsh. **118,411,286,386**) za bajeti, sawa na asilimia 52.5 ya Shilingi **bilioni mia mbili ishirini na tano mia sita sitini na tisa milioni mia nne hamsini na sita elfu mia nane sabini na tisa** (Tsh. **225,669,456,879**) zilizoidhinishwa. Kati ya hizo Shilingi **bilioni arobaini mia sita sabini na nane milioni mia sita na tano mia nane arobaini na sita (Tsh. 40,678,605,846**) ni mishahara ya watumishi na Shilingi Tsh. **Bilioni themanini na nne mia nane thelathini na tisa elfu mia mbili themanini na saba** (**Tsh. 84,890,939,287**) ni

kwa Matumizi Mengineyo ambapo fedha za maendeleo ni Shilingi **milioni mia tisa na tatu mia saba thelathini na mbili mia na nane kumi na nane (Tsh. 903,732,818**) zote zikiwa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kujiridhisha na mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa taasisi zilizo chini ya wizara hii, Kamati ilichambua mwenendo huo kwa kila Fungu na kuwianisha upatikanaji huo na Bajeti iliyoidhinishwa. Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa uwiano wa upatikanaji wa fedha ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge unatofautiana miongoni mwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Mfuko wa Mahakama, Fungu 40 umekuwa na uwiano mzuri kuliko taasisi nyingine. Mfuko huu hadi kufikia tarahe 31 Machi, 2015 ulipokea asilimia 65.54 ya Bajeti yake iliyoidhinishwa, wakati taasisi nyingine zilipokea pungufu ya asilima hiyo ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi iliyokuwa na asilima kidogo ya bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na taasisi nyingine ni Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria. Kiasi cha fedha zilizopatikana kwa Fungu hili ni asilimia 36.7 wakati taasisi nyingine zilipata zaidi ya asilimia hiyo ya bajeti

iliyoidhinishwa. Ili kuliwezesha Bunge hili kupata picha halisi, Kamati imeandaa Chati Na. 01 kwa madhumuni hayo.




**Chanzo:** ***Randama na Maelezo ya Waziri wa Katiba na Sheria yaliyowasilishwa kwenye Kamati***

**Mheshimiwa Spika,** kwa mchanganuo huu ni dhahiri kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa

ajili ya wizara hii hauridhishi hasa kwa fedha za miradi ya maendeleo. Hali hii inahitaji kufanyiwa kazi ili isijirudie kwa mwaka wafedha 2015/2016.

## 2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Ushauri huo ulilenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa Majukumu katika Ofisi hii. Kamati ilitaka kujiridhisha ni kwa kiasi gani maoni na ushauri wake ulizingatiwa na Serikali. Kamati ilibaini kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri wa kamati ulizingatiwa. Hata hivyo baadhi ya maoni na ushauri upo katika hatua za utekelezaji na mwingine haukuzingatiwa.

### 2.1.1 Maoni na ushauri wa Kamati uliotekelezwa na Serikali

**i) Ushauri kuhusu Tume ya Utumshi wa Mahakama kujengewa uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti kuongezeka kwa vitendo vya rushwa miongoni mwa watumishi wa mahakama.**

Ushauri huu umetekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya ili kuzimarisha ambapo Mikoa 8 pamoja na Wilaya zake ambayo ni Tabora, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Iringa, Pwani, Morogoro na Dodoma tayari zimekwishapewa mafunzo hadi sasa. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya shs. 184,220,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleea kutoa mafunzo kwa Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

ii) **Kutokana na uhaba wa fedha Serikalini na ukomo wa bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati inashauri Wizara kufanya utaratibu wa kuhamishia kiasi cha Shilingi Bilioni moja na Millioni mia nne (1,400,000,000/=) kutoka mfuko wa Mahakama mapema kwenda Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

Wizara imetekeleza agizo hili kwa barua Kumb. Na. AB 67/341/01 ya tarehe 06 Mei, 2014 kwenda kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, na kufuatiwa na uhamisho wa kiasi cha Shilingi 1,400,000,000 kutoka Fungu 40, Mfumko wa Mahakama, kwenda Fungu 12, Tume ya Utumishi wa Mahakama. Uhamisho huu uliongeza

ukomo wa bajeti katika Fungu hili kutoka Shilingi 2,871,716,000 hadi 4,271,716,000.

iii) **Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ijengewe uwezo katika kitengo cha mikataba kwa kuwapatia mafunzo Mawakili wa Serikali katika masuala ya mikataba ya mafuta na gesi ili kuhakikisha kuwa watendaji hao wanatumika ipasavyo kuishauri Serikali katika kuingia mikataba yenye tija kwa taifa kuhusu sekta hizo na nyingine.**

Kutokana na muundo wa ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa sasa eneo hili la mikataba limepewa hadhi ya kuwa Divisheni na siyo Kitengo, na liko chini ya uongozi wa Mkurugenzi akisaidiana na wakurugenzi wasaidizi wawili. Kila mwaka, Idadi ya mawakili wa serikali imekuwa ikiongezwa na sasa wapo mawakili 17. Ili kuboresha utendaji wa Divisheni ya Mikataba, Ofisi imekuwa ikiongezewa bajeti yake. Lengo likiwa ni kujenga uwezo wa kifedha na ujuzi kwa ajili ya eneo hili la mikataba.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na shirika la maendeleo la umoja wa Mataifa (UNDP) na Wizara ya

nishati na Madini iliandaa mafunzo ya kushughulikia mikataba ya gesi na mafuta(LING) kwa ajili ya kujenga uwezo wa mawakili wa serikali kuchambua na kujadili mikataba ya rasilimali gesi ili kulinda maslahi ya nchi. Mafunzo hayo yalishirikisha mawakili 32 kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Wizara ya nishati na Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji, Wizara ya fedha na wakala wa umeme Vijijini.

Chini ya Mradi Huu, Divisheni ya Mikataba ilitengewa bajeti ya shilingi 457,149,000 kwa ajili ya kupatiwa mafunzo watumishi waliopo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hadi Machi, 2015 kiasi cha shilingi 113,580,000 kimetolewa kuwapatia mafunzo ya kushughulikia mikataba ya gesi na mafuta

iv) **Kwa kuwa bado hakuna uelewa wa kutosha kwa wananchi kuhusu uwepo wa Tume na Kamati za Maadili za Mahakama pamoja na Majukumu yake, Kamati inashauri kuwa Elimu kuhusu uwepo wa Tume pamoja na majukumu yake iendelee kutolewa hasa vijijni ili kuwawezesha wananchi kuitumia kwa**

**kupeleka malalamiko wakiona kuna ukiukwaji wa maadili.**

Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 jumla ya shs. 110,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma kuhusu kuwepo kwa Kamati za Maadili ya Mahakimu za Mikoa na Wilaya. Aidha, Tume inatumia njia nyingine ikiwa ni pamoja na kuwasiliana na Wakuu wa Wilaya ambao ndiyo wenyeviti wa Kamati za Wilaya ili waweze kutoa elimu hii kwenye maeneo yao wakati wa mikutano na Wananchi. Pia yapo mawasiliano na Halmashauri yenye lengo la kuwaomba Madiwani kutoa elimu hii kwa wananchi katika maeneo yao. Hii itasaidia elimu hii kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa muda mfupi na kwa gharama kidogo

v) **Kwa kuwa Serikali imeendelea kuijengea uwezo Mahakama ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mahakama na kwa kuzingatia kuwa Mwasheria Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama, Kamati inashauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha**

**kuwa vyombo hivi vinafanya kazi kwa ufanisi katika kuhakikisha kuwa azma ya utoaji haki sawa na kwa wakati inafikiwa.**

Serikali inakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati kuwa maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Katika kutekeleza ushauri huu, Serikali kwa mwaka 2014/2015 ilitoa kibali cha ajira kwa watumishi 429 wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hadi machi 2015 tayari watumishi 321 wamesharipoti ofisini. Pia ofisi kwa mwaka 2014/2015 imetengewa Shilingi Bilion 5 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali Makao Makuu na Mikoani.

### 2.1.2Ushauri wa Kamati unaoendeea kutekelezwa

i) **Mahakama ipewe kibali cha kuajiri watumishi wengine wakiwemo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi sambamba na kuboresha maslahi ya Watumishi hao.**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mahakama ya Tanzania imepata vibali vya ajira kwa watuishi 1,010 wakiwemo Mahakimu hadi sasa nafasi 750

zimetangazwa na mchakato unaendelea kuwapata watumishi hao.

ii) **Kamati inashauri Serikali itenge fedha za ndani za kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili iweze kujenga ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Taasisi hii. Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.**

Katika kujenga uwezo wa Divisheni ya Mashtaka, Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi 429 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Hadi Machi, 2015 tayari watumishi 289 walikuwa wameripoti kwenye vituo vyao vya kazi na 140 zilizobaki zimetangazwa tena. taratibu za kuwapatia mafunzo zinafanyika.

iii) **Kamati ilielezwa kwamba Wizara ina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara iliomba kibali cha kuajiri watumishi 22 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 lakini hakikutolewa. Hivyo Kamati inashauri kwamba vibali**

**hivyo vitolewe ili kuijengea uwezo Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imeomba kibali cha kuajiri watumishi 15 ambapo nafasi 2 kati ya hizo zimejazwa bado nafasi 13 kibali kinafuatiliwa Utumishi.

**2.1.3Ushauri wa Kamati ambao haujatekelezwa**

i) **Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mawakili wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa.**

Serikali ilipokea ushauri wa Kamati, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ofisi ya mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa kiasi cha Shilingi bil.5 (5,000,000,000) za fedha za ndani za maendeleo ili kuanza ujenzi wa Ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi. Hadi mwezi machi kiasi hicho cha fedha hakijatolewa kutoka Hazina.Katika jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi.

ii) **Kutokana na upungufu na uduni wa Ofisi pamoja na vitendea kazi, Kamati inashauri hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kujenga majengo ya**

**Mahakama na kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa ili kuamsha ari ya utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa Mahakama**

Mahakama imekamilisha michoro (model courts) kwa ajili ya Mahakama Kuu, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto kubwa kuhusu upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo na hivyo kusababisha kukwama au kuchekewa kuanza kwa kazi zilizopangwa

iii) **Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Taarifa ya Mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.**

Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimeanza mashauriano kuhusu namna bora ya kuyafanyia kazi mapendekezo ya Taarifa ya Tume

**iv) Serikali itoe kiasi cha fedha inachodaiwa na RITA ili kuiwezesha kutekeleza wajibu wake katika mkataba wa ubia wa jengo la RITA Tower ili kuepukana na uwezekano wa riba kubwa kutokea kwa kuchelewa kulipa kiasi inachodaiwa**

Wakala katika mwaka wa fedha 2014/15 ilitenga kiasi cha Shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kulipa deni lake katika Mradi wa ujenzi wa jengo la RITA Tower kutokana na fedha inazodai kutoka Wizara ya Fedha, kiasi ambacho hakijatolewa hadi sasa. Ili kuhakikisha kuwa deni hilo linalipwa RITA imetenga kiasi cha Shilingi 5,000,000,000 kutoka katika makusanyo ya ndani katika makadirio ya bajeti ya mwaka 2015/2016 sambamba na kufanya mazungumzo na NSSF kuhusu namna ya kushughulikia suala hilo.


## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii na taasisi zilizo chini yake, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila Fungu kwa mafungu yote saba. Kwa upande wa Malengo na majukumu

yaliyowekwa, Kamati iliridhishwa mpango huo wa Wizara hii na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2015/2016 kama alivyowasilisha mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ulifanyika kwa kuhusianisha kiasi cha fedha inayoombwa na uzito pamoja na umuhimu wa malengo yanayowekwa kwa kila Fungu. Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwa bajeti katika Fungu 35 - Divisheni ya Mashitaka na Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria zitaongezeka kwa kiasi wakati Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali litakuwa na asilimia ya punguzo kubwa zaidi ya mafungu mengine ikilinganishwa na bajeti ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika**, sura nzima ya uwiano wa kupungua au kuongezeka kwa bajeti za Wizara na Taasisi zilizo chini yake inaonekana katika Chati Na. 02 ya Taarifa hii.




**Chanzo:** ***Randama zilizowasilishwa mbele ya Kamati***

## 4.0 MAONI NA USHAURI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

### 4.1 Tume ya Utumishi wa Mahakama - Fungu 12

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi wa Mahakama ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura 237, ikiwa na jukumu la kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume ya Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa Mahakama Kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha Kamati hizo kukaa na kuchunguza malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa Maadili na nidhamu za Watumishi wa Mahakama.

ii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iweke utaratibu madhubuti wa kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu uwepo wa Tume hiyo na Majukumu yake ili wananchi waweze kupeleka malalamiko pale wanabaini ukiukwaji wa maadili na nidhamu ya Watumishi wa Mahakama kwani si wananchi wengi wanaofahamu uwepo wa Tume hii.

iii) Serikali iendelee kuijengea uwezo wa kifedha na kirasilimali watu Tume ya Utumishi wa Mahakama ili

iweze kuwapatia Mafunzo watumishi watumishi wake kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

iv) Tume ya Utumishi wa Mahakama iimarishe udhibiti wa nidhamu kwa Mahakimu na Majaji ili kuepusha watendaji wa taasisi Muhimu ya Mahakama kuhusishwa na vitendo vya ukiukwaji wa Maadili ikiwepo kuhusishwa na vitendo vya rushwa jambo linaloipunguzia heshima Taasisi ya Mahakama mbele ya Jamii.

v) Tume iongeze juhudi za kuzijengea uwezo Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya zote nchini kwa kuzipatia mafunzo stahiki ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu.

**4.2 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Fungu 16**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali, hivyo Kamati inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji wake:-

i) Kutokana na ongezeko la kazi zilizosababishwa na kuongezeka kwa uhalifu nchini ,watumishi wa ofisi hii hasa mawakili wa Serikali hawawiani na ongezeko la

uhalifu, hivyo,Kamati inashauri Serikali kupitia Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha kuajiri watumishi wa kutosha ili kuwezesha ofisi hii kuhimili kasi ya ongezeko la uhalifu.

ii) Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi wa ofisi hii ukizingatia uzito na unyeti wa kazi wanazofanya kwa kuweka mazingira stahiki yatakayoleta motisha kwa watumishi ili kuongeza ari ya ufanisi wa utendaji kazi.

iii) Serikali iongeze kasi ya kuimarisha ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuitengea bajeti ya kutosha, kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati na kuipa vitendea kazi vya kisasa vinavyotosheleza mahitaji pamoja na kujenga ofisi za kutosha kwa ajili watumishi wa ofisi hii ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

iv) Serikali itilie maanani suala la kuwajengea uwezo na ujuzi watumishi wa ofisi hii kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika Nyanja mbalimbali kulingana na taaluma zao hasa katika nyanja za makosa ya kimtandao ili kuwawezesha kutimiza majukumu yao kwa ufanisi.

### 4.3 Divisheni ya Mashitaka (DPP) - Fungu 35

**Mheshimiwa Spika,** Divisheni ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa kupitia Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake kwa ajili ya kutekeleza jukumu muhimu katika Taifa letu la kuendesha Mashtaka na kuratibu kazi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi kama yalivyoainishwa na Katiba na sheria zingine. Kutokana na umuhimu huo, ili kuimarisha na kuboresha Divisheni hii, Kamati inaushauri kama ifuatavyo:-

i) Kwa kuwa kumekuwa na upanuzi wa maeneo ya kiutawala kwa kuongeza mikoa na wilaya hali ambayo imelazimu Ofisi hii kufungua ofisi katika maeneo na hivyo kusababisha kupanuka kwa majukumu katika ngazi hizo, ni vema Serikali ikatenga bajeti ya kutosha inayolingana na mahitaji halisi ya ongezeko na upanuzi wa majukumu ya Ofisi na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya ofisi hii zinatolewa kwa wakati.

ii) Kutokana na kuongezeka kwa wimbi la uhalifu wa makosa ya jinai kama vile utakatishaji fedha/mali haramu, matumizi ya vyombo vya usafiri vya umma

ikiwa ni pamoja na kusafirisha dawa za kulevya, silaha, milipuko, nyara za Serikali na usafirishaji haramu wa binadamu, Kamati inashauri Serikali iongeze jitihada za kuwajengea uwezo Watumishi wa Ofisi hii hasa mawakili wa Serikali ili waweze kukabiliana na wimbi hili la uhalifu.

iii) Ili kuhakikisha usalama wa Mawakili wa Serikali kutokana na uhusika wao wa kushughulikia kesi zinazohusu wahalifu na mashauri ya mikataba, Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwajengea nyumba (quarters) katika eneo lenye usalama ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa haki na bila woga wowote kuhusiana na usalama wao.

iv) Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iendelee kudhibiti nidhamu ya Mawakili wa Serikali ili kuhakikisha kuwa Mawakili wanafanya kazi zao kwa nidhamu ya hali ya juu na wanajiepusha na vitendo vya rushwa na kuhakikisha kuwa Mawakili wanaobainika kujuhusisha na vitendo vya rushwa wanachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwepo kuwafukuza kazi.

v) Serikali iimarishe Mfumo wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuweka mfumo wa kisasa wa utunzaji wa kumbukumbu za kisheria utakaotumia TEKNOHAMA ili kuwezesha huduma za kisheria zinatolewa kwa ufanisi katika ngazi zote na kuimarisha mfumo wa matumizi ya kompyuta katika uendeshaji wa Mashauri nchini.

## 4.4 Mfuko wa Mahakama - Fungu 40

**Mheshimiwa Spika,** Mahakama ni mojawapo ya Mihimili mitatu ya Dola yenye jukumu kubwa la kutafsiri Sheria na Kutolea uamuzi mashauri mbalimbali yanayowasilishwa kwake na wananchi. Kwa mujibu wa Ibara ya 107 (A),(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mahakama ndicho chombo cha mwisho cha kusimamia na kutoa uamuzi wa mwisho katika masuala ya utoaji Haki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuthamini juhudi kubwa zinazofanywa na Mahakama ya Tanzania katika kupunguza mlundikano wa mashauri na hivyo kukuza imani kwa Wananchi na hivyo kuwawezesha kukitumia chombo hiki kikamilifu ili waweze kupata haki zao kwa mujibu wa Sheria**.**Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 hadi

kufikia machi 2015 Mahakama imesikiliza na kutolea uamuzi jumla ya mashauri 179,962. Hii ni hatua kubwa na ya kupongezwa na kila mwananchi anayependa haki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na kasi hii na inaamini kwamba kama kasi hii ikiendelea Mahakama inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi, Kamati inashauri kama ifuatavyo ili kuboresha na kuimarisha utendaji wa Mhimili huu:-

i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama zinatolewa zote na kwa wakati Ili kuhakikisha shughuli zinazopangwa na Mahakama zinatekelezwa kikamilifu.

ii) Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itoe kibali cha ajira kwa Makahama ili kuiwezesha Mahakama kukabiliana na upungufu wa watumishi wakiwemo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

iii) Kwa kuwa baadhi ya Makao Makuu ya Mikoa bado hayana Mahakama Kuu, na Mahakama nyingi zilizopo sasa hasa Mahakama za Mwanzo zimechakaa hivyo

kuhitaji ukarabati mkubwa na wa haraka, Kamati inashauri Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 zitolewe zote na kwa Wakati ili kuwezesha Mahakama hizo kujengwa na kukarabatiwa kwa lengo la kujenga mazingira mazuri ya utoaji haki kwa watendaji wa Mahakama na Wananchi kwa ujumla.

iv) Serikali iboreshe Maslahi na mazingira ya kufanyia kazi ya Watendaji wa Mahakama ili kuwapa motisha Watendaji hao na kuhakikisha kuwa wanajiepusha na vitendo vya rushwa kwani maslahi yasiyoridhisha ni kichocheo kimojawapo cha rushwa.

v) Serikali ihakikishe inaboresha Mahakama za Mwanzo zote nchini kwa kuzipatia vitendea kazi kama kompyuta, meza, usafiri na mawasiliano. Kupatikana kwa vitendea kazi hivyo kutasaidia kuleta ufanisi katika utendaji wa Mahakama za Mwanzo.

vi) Viongozi wa Mahakama akiwemo Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi ,Majaji Wafawidhi, Wasajili na Mahakimu Wafawidhi waongeze juhudi za kutembelea Mahakama za ngazi mbalimbali nchini ili kubaini changamoto zinazozikabili na kuzitatua kwa Wakati.

vii) Pamoja na jitihada kubwa zilizofanyika katika kumaliza mrundikano wa Mashauri, Kamati inashauri Mahakama kuongeza jitihada zaidi ili kumaliza kabisa tatizo na mrundikano wa Mashauri nchini.

viii) Mahakama iendelee kuimarisha usafiri wa Umma kwa ajili ya Watumishi wa Mahakama ili kurahisisha usafiri wa Watendaji hao na kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mahakama nchini.

ix) Kwa kuwa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara ilianzishwa kwa lengo la kuharakisha mashauri ya kibiashara ili kuhakikisha kuwa shughuli za uwekezaji haziathiriwi na ucheleweshaji wa mashauri hayo, na kwa kuwa Sera ya Mahakama ni kuhakikisha kuwa Majaji hawakai katika kituo kimoja kwa zaidi ya miaka mitatu ni vyema Mahakama ikahakikisha kuwa utaratibu wa kuhamisha Majaji katika divisheni hiyo unafanyika vizuri pasipo kuathiri mashauri mbalimbali yanayoendelea kusikilizwa na kuhakikisha kuwa Majaji wa Divisheni hiyo hawahamishwi wote kwa wakati mmoja ili kuhakikisha uzoefu unaoendelezwa na kurithishwa kwa majaji wageni. Aidha, Mahakama ihakikishe kuwa Majaji wa Divisheni hii wanaohamishwa wanapewa muda wa kutosha ili

kukamilisha kuandika hukumu na kuzisoma kabla hawaripoti katika vituo vipya wanakohamishiwa.

### 4.5 Wizara ya Katiba Na Sheria – Fungu 41

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo chombo kikuu cha Serikali katika masuala yote ya kisheria katika nchi ikiwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kunakuwa na utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuwepo kwa mfumo wa sheria unaotoa fursa sawa kwa watu wote katika jamii ili kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa Sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu. Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii na ili iendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

i) Kwa kuwa kuna taasisi nyingi zinazotoa msaada wa sheria kwa wananchi wasiojiweza nchini, Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria iandae muswada wa Sheria utakaounda chombo mahsusi pamoja na mambo mengine kitakachokuwa na jukumu la kutoa msaada wa sheria na kuratibu

utaratibu mzuri wa utoaji huduma ya Msaada wa Kisheria ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hii na kuwanufaika walengwa katika kulinda na kutetea haki zao.

ii) Wizara ya Katiba na Sheria iendelee kuratibu na kusimamia kikamilifu utendaji wa taasisi zilizo chini yake ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza wajibu wao kikamilifu.

iii) Kwa kuwa ufaulu wa wanafunzi wa shule ya sheria kwa vitendo umekuwa si wa kuridhisha,Kamati inashauri Serikali kusimamia kikamilifu Taasisi hii kwa kufanya utafiti ili kubaini chanzo cha tatizo hili na kulitafutia ufumbufu wa kudumu.

iv) Kwa kuzingatia majukumu muhimu ya wizara hii,Kamati inashauri Serikali iwezeshe wizara hii kwa kuitengea bajeti muafaka na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati,kuipa rasilimaliwatu na vitendea kazi vya kisasa ili kuimarisha wizara hii kwa lengo la kuimarisha mfumo wa sheria nchini na kufikia azma ya haki sawa na kwa wakati.

v) Kwa kuwa taasisi nyingi za  wizara ya Katiba na Sheria ofisi zake zipo katika majengo ya kupanga hali

inayoisababishia wizara kutumia gharama kubwa kwa ajili hiyo, hivyo, Kamati inashauri Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga majengo yake ili kuepuka gharama za upangaji wa ofisi hizo

vi) Kwa kuwa Kamati wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ilielezwa kuwa wizara inakabiliwa na malimbikizo ya madeni ya watumishi na wazabuni,Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye uhakiki wa madeni hayo na kuyalipa kwa wakati kwa lengo la kuimarisha ari ya watumishi hao na wazabuni ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### 4.6 Tume ya Kurekebisha Sheria- Fungu 59

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria ni Taasisi ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoanzishwa kwa mujibu Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura 171. Majukumu ya Tume ni kufanya mapitio ya Sheria Mbalimbali, kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo kisha kuyawasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria. Waziri

wa Katiba na Sheria baada ya kupokea mapendekezo hayo huyawasilisha Bungeni kwa ajili ya utunzi wa Sheria au kuzifanyia mabadiliko Sheria zinazokuwa zina mapungufu katika kuhakikisha kuwa Sheria za nchi zinaenda sanjari na mazingira ya sasa katika kudumisha utawala wa Sheria na usimamizi wa Haki nchini.

Ili kuboresha utendaji kazi wa Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

i) Kwa kuwa Tume ya Kurekebisha sheria hufanya utafiti wa sheria mbalimbali kwa kutumia muda,rasilimali watu na fedha kisha kuandaa mapendekezo na kuwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa ajili ya kufanyia kazi mapendekezo hayo,hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa tafiti hizi hazifanyiwi kazi kwa wakati,Kamati inashauri Serikali kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Tume hii kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yanayotolewa ili kuboresha sheria za nchi yetu ziweze kuendana na wakati.

ii) Kwa kuwa kazi ya kufanya utafiti kuhusu sheria mbalimbali hufanywa na wizara/taasisi nyingine nchini nje ya Tume ya kurekebisha Sheria, hivyo kusababisha kazi zinazofanana (duplication of work)

na kutumia rasilimali na muda, Kamati inashauri Serikali iweke mfumo thabiti wa namna ya wizara na taasisi zinazofanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali kusimamiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria kwani ndiyo yenye jukumu kisheria la kufanya tafiti.

iii) Tume iendelee kufanya tafiti kuhusu sheria mbalimbali ambazo kutokana na mabadiliko ya kujamii, kisiasa na kiuchumi zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziweze kuendana na wakati.

iv) Serikali iendelee kuijengea uwezo Tume ya kurekebisha Sheria kwa kuipatia fedha za kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 4.7 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Fungu 55

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni idara huru ya Serikali ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake ikisomwa pamoja na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura 391. Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba.

Jukumu kubwa la Tume hii ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

i) Kwa kuwa fedha zinazotengwa kila mwaka wa Fedha zimekuwa hazikidhi mahitaji halisi ya Tume ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Tume, Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

ii) Kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala utolewaji wake kutoka Hazina umekuwa si wa kuridhisha hali inayokwamisha utekelezaji wa majukumu yake,matharani fedha iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Tume kwa mwaka wa 2014/ 2015 kiasi cha shilingi 6,734,370,800/= hadi kufikia May,2015 ni shilingi 3,119,015,975 tu ndicho kilitolewa na Hazina sawa na asilimia 34.Kwa mazingira haya Kamati inashauri Serikali ihakikishe fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Tume zinatolewa kwa wakati ili iweze kutimiza azma yake ya kujenga jamii ya watu wanaojali haki na utamaduni

unaoheshimu,kulinda,kutekeleza na kudumisha haki za binadamu na misingi ya utawla bora.

iii) Kutokana na umuhimu wa ofisi kwa ustawi wa Taifa letu,Kamati inashauri Serikali ichukue hatua madhubuti za kufungua ofisi za Tume katika kila mkoa ili kusogeza huduma hii muhimu kwa wananchi na kuwaondolea adha ya kufuata huduma hii Dar es salaam,Mwanza,Lindi na Zanzibar pekee.

iv) Kwa kuwa Tume inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile kompyuta,samani za ofisi na magari,Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuijengea uwezo Tume hii kwa kutenga fedha za kununua vitendea kazi vya kisasa.

**4.8 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*Registration, Insolvency and Trusteeship Agency*-RITA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Usajili ,Ufilisi na Udhamini (RITA) ni idara ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria yenye jukumu la kusajili na kuweka kumbukumbuku muhimu za maisha ya binadamu nchini kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa idara hii kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuimarisha na kuboresha idara hii:-

i) Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuiwezesha Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini **(RITA)** ili ktekelezaji wa majukumu yake,hata hivyo Kamati inaendelea Kushauri Serikali kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya wakala huu zitolewe kwa wakati ili iweze kutekeleza mipango iliyopangwa kwa mwaka husika.

ii) Pamoja na zoezi la utoaji elimu kwa wananchi kuhusu majukumu na umuhimu wa wakala huu kufanyika, Kamati imebaini kuwa bado elimu hiyo haijaeleweka kikamilifu kwa wananchi,hivyo Kamati inashauri Serikali kupitia wakala huu iongeze kasi ya utoaji elimu hasa vijijini ili kuwawezesha wananchi wengi kujisajili hivyo kuliwezesha Taifa kuwa na takwimu sahihi kwa ajili ya kupanga na kutekeza mipango ya maendeleo kwa wanachi wote.

iii) Kwa kuwa Serikali imeanza mchakato wa kutunga Sheria ya Usajili na Sheria Ufilisi nchini, Kamati inashauri mchakato huo kuharakishwa na mswaada huo uletwe Bungeni kwa lengo la kutungwa sheria hizo ili utekelezaji wake uwanufaishe wananchi.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt Asha- Rose Migiro, (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Ummy A.Mwalimu (Mb), Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, George Mcheche Masaju, (Mb), na Naibu Mwansheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George M. Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu sekta ya sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo**:-**

1) Mhe. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) - Mwenyekiti
2) Mhe. Gosbert Begumisa Blandes, (Mb) - M/Mwenyekiti
3) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu,(Mb) - Mjumbe
4) Mhe. Nimrod Elirehema Mkono,(Mb) - Mjumbe
5) Mhe. Halima James Mdee, (Mb) - Mjumbe
6) Mhe. Fakharia Khamis Shomar,(Mb) - Mjumbe
7) Mhe. Nyambari C.M Nyangwine, (Mb) - Mjumbe
8) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, (Mb) - Mjumbe
9) Mhe. Felix Francis Mkosamali, (Mb) - Mjumbe
10) Mhe. Rukia Khasim Ahmed, (Mb) - Mjumbe
11) Mhe. Mustapha Boay Akunaay,(Mb) - Mjumbe
12) Mhe. Ramadhan Haji Saleh, (Mb) - Mjumbe
13) Mhe. Tundu Antipas Mughwai Lissu,(Mb) - Mjumbe
14) Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina,(Mb) - Mjumbe
15) Mhe. William Mganga Ngeleja, (Mb - Mjumbe
16) Mhe. Ali Khamis Seif,(Mb) - Mjumbe
17) Abdallah Sharia Ameir,(Mb) - Mjumbe
18) Mhe. Mariam R. Kasembe,(Mb) - Mjumbe
19) Mhe. Zahra Ali Hamad, (Mb) - Mjumbe
20) Mhe,Shamsi Vuai Nahodha, (Mb) - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, Ndugu Charles Joseph Mloka,Mkurugenzi wa Idara ya Kamati na Ndugu Athuman Brambath Hussein kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo, ndugu Maria Mdulugu na ndugu Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

**Mheshimiwa spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mhe. Jasson Samson Rweikiza (Mb)

Mwenyekiti

**KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA**

20 Mei, 2015